

**Somo: KILA MTEULE ANA JIONI YAKE KATIKA  
MAISHA YAKE YA WOKOVU**

**Maandiko: ESTA 4: 1 – 4, MARK. 6: 45 – 52**

**1. UTANGULIZI:**

Ninapozungumza jioni namaanisha kwamba kila mteule ana wakati ambao anaona wokovu ni mgumu sana kutokana na changamoto anazokutana nazo katika maisha yake baada ya kuokoka; anakabilia na mambo magumu ambayo hayana **suluhu, hayana njia ya kuyatatua, analia, anaomba, anafunga, anakesha, anaishi maisha ya dhiki na taabu, na kipindi hiki Yesu naye anajifanya kama haoni, hadi atakapona mteule huyo anapiga yowe ya kuhitaji msaada wake kweli kweli.**

- Katika kipindi kama hiki usipokuwa makini, hiki ndicho kipindi unachoweza kumkosea Mungu au kuwa rafiki sana na Mungu kutegemea na maneno utakayokuwa unayasema wewe mwenyewe au mbele za watu!!! **Ayub. 42: 7 -9;** Katika kipindi kama hiki Yesu anaweza kutukaribia ili azungumze nawe kama mwanadamu wa kawaida na unaweza **ukamfokea** au **ukamkunja uso. Luk.24:13-35.**

**2. Swala la Yesu kujifanya kama haoni shida yako lengo lake ni kutaka kuujua hasa moyo wako na maamuzi yako hasa. Mwanz. 42: 1-38 halafu soma tena 43: 1-34 halafu 44 yote na mwisho Mwanzo 45:1-28 linganisha na Mtume Paulo anavyosema katika 1Kor. 9: 19 – 24 na uone Yesu alivyojifanya kuwa hana utukufu wowote. Fillip. 2: 5 – 8; Ebr. 2: 14 – 18.**

- Matokeo ya ndugu zake na Yusufu baada ya kueleza kweli yote, ndipo Yusufu alipojidhihirisha kwao na kisha akawatendea mema ya ajabu na jioni yao ikageuka kuwa asubuhi *Mwaz. 46: 28-34, 47:7 – 12.*

3. Nimetangulia kuwambia kwamba Yesu ana tabia ya **kujifanya** kama haoni jioni ya mtu hadi mtu Yule atakapopiga **YOWE** ya kuhitaji msaada kutoka kwake, na ndugu zangu kama utashupaza shingo ukakaa kimya na shida yako, pamoja na Yesu kuziona taabu zako na dhiki zako, ataendelea kujifanya kama hazioni; nasema kweli mbele zenu kwamba kama hutajizoeza kupiga **yowe** mbele za Mungu kama Mordekai na Esta walivyopiga yowe, tutaendelea kuteseka na wakati mwingine hata kufa kabisa na shida zetu. *Esta 4: 1 – 4, 12 – 17, 6: 1 – 14, 8: 1 – 8; Soma pia 1Samwl. 1: 9 -20, 2:8.*

**Elewa kwamba:-ukubwa wa jioni yako (jaribu lako/tatizo lako ulilonalo) siyo sawa na ukubwa wa ushindi ulio mbele yako!!! Wala ukubwa pamoja na vitisho vyote vya ibilisi siyo sawa na ukubwa wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyefufuka kwa ushindi mkubwa. Ayub.42:7-17.**

**Note:** Yesu anatengeneza Tiba ya ugonjwa kabla hata hujaugua, hii ndiyo tofauti yake na wanadamu – Hebu kila mmoja katika jioni yake aliyo nayo apige Yowe kwake leo ili aone matokeo makubwa. **Amina.**

**Na**  
**Ask. Dr. L. M. Mwizarubi**  
**29/05/2022**